



WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA
SHIRIKA LA VIWANGO TANZANIA



ISO 9001:2015 Certified

Mwanachama wa Shirika la Viwango la Kimataifa (ISO), Codex Alimentarius Commission (WHO/FAO) na Wakala wa ISO na Mashirika ya Viwango ya Mataifa mbalimbali

TAARIFA KWA UMMA KUHUSU MTANZANIA ALIYEBUNI BAJAJ

Dar es Salaam, 30 Aprili, 2024

Hivi karibuni, kumekuwepo na taarifa inayosambaa kuhusu Mtanzania aliyebuni chombo cha usafiri cha matairi matatu maarufu kama "Bajaj" ambayo inaelezea TBS kuikataa sababu ya kuzidi urefu.

TBS inapenda kuujulisha umma kuwa ilifanya ukaguzi wa *Bajaj* husika mwaka 2018 kulingana na matakwa ya kiwango cha kitaifa, yaani "*TZS 1231-2:2010 Motorcycles for general use — Part 2: Specifications for three wheeled motorcycles*" ambapo urefu ilikuwa ni moja ya mapungufu yaliyoonekana katika *Bajaj* hiyo. Mapungufu mengine yaliyoonekana ili kufikia vigezo vya usalama na ubora ni kama yafuatayo:

- a) Kuwa na kipenyo cha kukatia kona kikubwa (turning radius) ambacho kinasababisha *Bajaj* kukata kona kubwa isiyolingana na urefu wa *Bajaj* kwenye barabara za kawaida, hivyo kuathiri urahisi wa kutumika kwake sambamba na vyombo vingine vya moto hasa kwenye maungio ya barabara na wakati wa kugeuka;
- b) Usukani kuwa mgumu na hivyo kusababisha kushindwa kukata kona;
- c) Tenki la mafuta kuwekwa karibu na betri jambo ambalo huweza kusababisha moto;
- d) Kutotumia vioo vyenye karatasi katikati (laminated and toughened glass) ambavyo huzuia abiria kujeruhwa na kioo endapo ajali itatokea;
- e) Mfumo wa breki kutokuwa imara; na
- f) Kuwaka kwa ugumu na kwa kuchelewa (hard start).

Hata hivyo, TBS huwa ina utaratibu wa kuhuisha viwango na kiwango husika kilihuishwa mwaka 2023 na kuruhusu urefu zaidi wa *Bajaj* kuendana na mazingira na matumizi ya hapa nchini.

Baada ya ukaguzi, wataalam wa TBS, NIT na SIDO walikaa na mtengenezaji na kumshauri kufanya marekebisho katika maeneo yenye mapungufu, ambapo mpaka sasa hajaweza kurekebisha na kukidhi matakwa ya kiwango husika ili kulinda usalama wa mwendeshaji pamoja na abiria.

Vilevile, mtengenezaji alishauriwa na SIDO kuhusu fursa zilizopo katika Shirika hilo ikiwa ni pamoja na uatamizi (incubation) wa wazo lake na pia mifuko ya mikopo kwa ajili ya wajasiriamali wadogo. Hata hivyo, juhudzi za kumtafuta mtengenezaji zimekuwa zikifanywa mara kwa mara bila mafanikio.

Shirika linaendelea kumsisitiza mtengenezaji kufanya marekebisho yaliyoainishwa ili *Bajaj* hiyo iweze kuwa salama kwa matumizi barabarani.

Aidha, wabunifu wengine wa vyombo vya moto wanaaswa kushirikiana na TBS kuanzia hatua za awali za ubunifu ili kuhakikisha vyombo hivyo vinakidhi matakwa ya viwango.

Imetolewa na:

Gladness H Kaseka
MENEJA UHUSIANO NA MASOKO

TBS MAKAO MAKUU
 Shirika la Viwango Tanzania
 Barabara ya Sam Nujoma /
 Morogoro, Ubungo, Dar es Salaam
 S. L. P. 9524
DAR ES SALAAM, TANZANIA
 Simu Na: +255 22 245 0298/
 +255 22 245 0206
 Nukushi: +255 22 2450959
 Namba ya Simu Bila Malipo: 0800110827
 Barua pepe: info@tbs.go.tz
 Tovuti: <http://www.tbs.go.tz>
 Barua pepe kwa ajili ya malalamiko ya
 wateja: malalamiko@tbs.go.tz
 Twitter: TBS_Tanzania
 Instagram: tbs_Viwango

TBS KANDA YA KATI
 Jengo la Kambarage
 S. L. P. 2956
DODOMA,
TANZANIA
 Simu Na:
 +255 26 2520310

TBS KANDA YA ZIWA
 Jengo la NSSF,
 Ghorofa ya 3
DODOMA,
TANZANIA
 Simu Na:
 +255 26 2520310

TBS KANDA YA KASKAZINI
 Jengo la NSSF (Mafao
 House), Ghorofa ya 2
 S. L. P. 2399
MWANZA,
TANZANIA
 Simu Na:
 +255 28 2505044

TBS KANDA YA NYANDA ZA JUU KUSINI
 Jengo la NHIF,
 Ghorofa ya 7
 S. L. P. 1674
ARUSHA,
TANZANIA
 Simu Na:
 +255 27 2520143

TBS KANDA YA KUSINI
 Jengo la MTUWASA
 S. L. P. 1396
MTWARA,
TANZANIA
 Simu Na:
 +255 25 2502848

TBS KANDA YA MAGHARIBI
 Jengo la NSSF (Mafao
 House), Ghorofa ya 2
 S. L. P. 1276
KIGOMA,
TANZANIA
 Simu Na:
 +255 23 2334477

+255 28 2804023